

**Kutengeneza Mambo Yaliyopungua  
(To Set In Order The Things That  
Are Lacking)**

**Na**

**John Kombo**

# **Kutengeneza Mambo Yaliyopungua (To Set In Order The Things That Are Lacking)**

**Na**

**John Kombo**

**March 14, 2013**

# Kutengeneza Mambo Yaliyopungua

“Kwa sababu hii nalikuacha Krete, ili uyatengeneze yaliyopunguka na kuweka wazee katika kila mji kama vile nilivyokuamuru.” (Tit. 1:5).

Kulingana na jinsi ujumbe huo kwa Tito unavyohusu hapo juu kutoka katika Tit. 1:5, mara zote kuna *“mambo yanayopunguka”* kwamba sisi watumishi wa Bwana wetu Yesu Kristo tunapaswa kufanya kazi ili kuyatengeneza. Yakiachwa bila kuyatengeneza kila kitu kitaenda vibaya.

Wakti Mtume Paulo alipokuwa analala, watu wa Makedonia walimjia katika maono na kumuomba, *“Njoo Makedonia na utusaidie”* (Mdo. 16:9).

Msaada ambao mtu alihitaji haikuelezwa, lakini Paulo alitambua kwamba msaada aliopaswa kutoa ilikuwa ni injili (Mdo. 16:10). Paulo alifanya haraka. Biblia inasema asubuhi na mapema alikuwa akichunguza maandiko kwa ajili ya Makedonia.

Katika maswala kama kwenda kuhubiri injili, Paulo hakupoteza wakati isipokuwa kama mazingira hayakuruhusu kufanya hivyo. Alionya kuhusu kutokutumia nafasi iliyopo. Alisema, *“Basi angalieni sana jinsi mnavyoenenda, si kama watu wasio na hekima bali kama watu wenye hekima; mkiukombo wakati kwa maana zama hizi ni za uovu.”* (Efe. 5:15,16)

Hataiyo katika Galatiamambo yalikuwa hayaendi vizuri wakati Paulo aliporudi. Hatufahamu kwa hakika ni muda gani alikaa bila kurudi au kumtuma mtu kama alivyofanya kwa kumtuma Tito Krete.

Lakini yote kwa yote hiki ndicho alisema alipofika Galatia, *“Nastaajabu kwa kuwa mnamwacha upesi hivi yeye aliyewaita katika neema ya Kristo, na kugeukia injili ya namna nyingine.”* (Gal. 1:6). Chochote kilichokuwa kinatokea Galatia kimeelezwa vizuri na Paulo; hakikuwa kizuri. Aliendelea, *“Wala si nyingine lakini wapo watu wawataabishao na kutaka kuigeuza injili ya Kristo.”* (ms. 7).

Ilitokea kipindi cha Paulo; bado pia inatokea leo. Swali ni, tunajali? Ni roho ngapi za watu zinaangamia kila siku katika weusi wa dhambi? Tunajali kwa kiwango gani kwamba roho zinapotea? Inatuhusu mara ngapi kwamba mamilioni hawajui chochote kuhusu Yesu na kanisa lake? Wengi wanadai kwamba wanamfahamu Yesu lakini hawajui kuhusu kanisa lake. Hawafahamu kwamba huwezi kutenganisha Yesu na kanisa lake. Hawajui dhamani ya kanisa lake, kwamba alilinunua na damu yake mwenyewe (Mdo. 20:28) kuna mchanganyiko hata kwa wale walioko katika kanisa la Bwana. Wanafundisha injili nyingine hasa katika meza ya Bwana. Wapo wale wanaosisitiza katika matumizi ya vikombe vingi. Hapa Kenya ni wengi. Biblia iko wazi, Yesu mwenyewe,

alipokuwa anaanzisha meza ya Bwana, “Alitwaa kikombe akakibariki akisema kikombe hiki ni agano jipya katika damu yangu, nyweni nyote katika hiki.” (Luka 22:17). Ni nani atatengeneza mambo yaliyopunguka? Ni wewe na mimi. Tunamhitaji kila mmoja wetu katika hili. Hatujachelewa isipokuwa tukijitoa sisi na vitu vyetu.

Kumbuka, siku moja ya hukumu mamilioni na mabilioni ya watu ambao hajafundishwa watamuona Mwokozi katika dhambi. Kama Bwana angetuuliza, “kwanini?” jibu sahihi itakuwaje, “hawakufundishwa na wakatotea kwa sababu hatukujali?”

**Ndoto ya Mungu** ni, “Hili ni zuri nalo lakubalika mbele za Mungu Mwokozi wetu; ambaye hutaka watu wote waokolewe na kupata kujua yaliyokweli. (1 Tim. 2:3-4)

Ni nani atafanya **Ndoto ya Mungu** kuwa kweli? Tena, wewe na mimi tunaifanya.

Ndugu, wapendwa njooni Nakuru Kenya na mtusaidie (Mdo. 16:9). Mtusaidie kuwageuza waliopotea kwa Kristo. Tusaidie kurudisha kanisa la Kristo, kanisa la Biblia. Mtusaidie kuwasaidia wengine pia (2 Tim. 2:2)

Mtusaidie ili kuwasaidia wengine warudi katika ibada ya kweli, kwa kutumia kikombe kimoja badala ya vikombe vingi, kama inavyofanywa na wengi wanaojiita “makanisa ya Kristo Kenya.

Labda kauli ya Paulo kiuhalisia inaweza kuwa na himizo kwetu, aliandika, “*hivyo tukiona tuna huduma hii, kama tunavyopata neema hatufi moyo.*”

Mungu awabariki

Wenu kwa sababu ya Kalvari

John Kombo Nandwa

Kanisa la Kristo Barut







